

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU



**MWONGOZO WA UANZISHAJI NA UENDESHAJI WA NYUMBA ZA UPATAJI  
NAFUU TANZANIA BARA**



Imeandaliwa na:  
Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya  
S.L.P 80327  
SIMU: 2152532  
NUKUSHI: 2152820  
DAR ES SALAAM

## **DIBAJI**

Nchi yetu imeendelea kukabiliwa na ongezeko la matumizi ya dawa za kulevya hasa katika kipindi cha miongo miwili iliyopita. Vijana ndilo kundi kubwa ambalo limeathirika zaidi na matumizi hayo na idadi yao inaongezeka siku hadi siku. Ili kukabiliana na ongezeko la idadi ya watumiaji, wadau mbalimbali walianzisha Nyumba za Upataji Nafuu (*Sober Houses*). Nyumba hizo zilianzishwa kwa lengo la kutoa huduma za upataji nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya.

Uanzishaji na uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu ulikuwa na changamoto nyingi hasa kutokana na kutokuwepo kwa mwongozo. Serikali kwa kutambua kutokuwepo kwa taratibu za uanzishaji na uendeshaji wa nyumba za upataji nafuu, imetoea mwongozo maalum wa kukabiliana na changamoto hiyo.

Mwongozo huu unaainisha vigezo vyta uanzishaji na uendeshaji wa huduma ya Nyumba za Upataji Nafuu Tanzania Bara. Wadau wanaoendesha na wanaokusudia kuanzisha Nyumba za Upataji Nafuu wanawajibika kutumia mwongozo huu ili kuimarisha utoaji huduma.

## **OFISI YA WAZIRI MKUU**

## **SHUKRANI**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta inathamini mchango wa wataalam mbalimbali waliohusika kutayarisha Mwongozo huu. Wataalam hao ni pamoja na Dkt. Norman Sabuni (MoHCDGEC), Dkt. Frank Masao (MNH), Dkt. Nelson Mabruki (IMC), Dkt. Cassian Nyandindi (DCEA), Dkt. Omary Ubuguyu (MNH), Mhandisi Jotham G. Mwakalinga (MoHCDGEC), Mahmoud Ibrahim Mussa (CNCDCCZ), Salome M. Mbonile (DCEA), Fatma Juma Mussa (Sober ya Wanawake Zanzibar), Dkt. Syangu Mkony (DCC), Amani Msami (DCC), Yovin Ivo (DCC), Alois Ngonyani (DCC), Suleiman Mauly (THPS), Frank Assenga (DFT), Nuru Salehe (PEDDEREF) na Al-Karim Bhanji (LHRO).

Vilevile, Mamlaka inatoa shukrani za dhati kwa Taasisi za TACAIDS, *Voice of Sober Houses* (VSH), Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, Asasi ya Changamoto ni Matumaini na Tume ya Kikristu ya Huduma za Jamii ya Tabora kwa mchango wao wa maoni ambayo yamefanikisha kuandaliwa na kukamilika kwa Mwongozo huu muhimu katika ustawi wa jamii yetu.

## **MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

## **YALIYOMO**

SHUKRANI.....	ii
YALIYOMO.....	iii
VIFUPISHO.....	v
MISAMIATI.....	vii
1 UTANGULIZI.....	1
1.1 Matumizi ya Dawa za Kulevyta Nchini .....	1
1.2 Athari za Matumizi ya Dawa za Kulevyta.....	1
1.3 Mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevyta nchini .....	2
1.4 Nyumba za Upataji Nafuu .....	2
1.4.1 Historia ya Nyumba za Upataji Nafuu Nchini .....	2
1.4.2 Umuhimu wa Mwongozo wa Nyumba za Upataji Nafuu.....	3
1.4.3 Kanuni za kuzingatiwa katika Nyumba za Upataji Nafuu .....	3
2 VIGEZO VYA UANZISHAJI NA UENDESHAJI WA NYUMBA ZA UPATAJI NAFUU.....	3
2.1 Miundombinu na Vifaa .....	3
2.2 Watoa huduma .....	5
2.3 Aina za huduma zinazotolewa .....	5
2.3.1 Huduma ya saikolojia – Jamii ( <i>phychosocial services</i> ) .....	5
2.3.2 Huduma ya kwanza .....	6
2.3.3 Huduma ya rufaa .....	6
2.3.4 Chakula na malazi .....	6
2.4 Usalama na dharura.....	6
2.5 Utupaji taka.....	7
3 UANZISHAJI NA UENDESHAJI WA NYUMBA ZA UPATAJI NAFUU .....	7
3.1 Umiliki .....	7
3.2 Ithibati ya uanzishwaji wa Nyumba za Upataji Nafuu.....	7
3.3 Utaratibu wa kupata Cheti cha idhini .....	8
3.4 Utaratibu wa kufutiwa utoaji huduma .....	8
3.5 Kusitisha utoaji huduma kwa hiari.....	8

3.6	Uongozi katika Nyumba ya Upataji Nafuu.....	8
3.7	Utaratibu wa kijiunga na nyumba za upataji nafuu .....	9
3.8	Usimamizi Shirikishi na Uhakiki wa Ubora wa Huduma.....	9
3.9	Kuunganishwa na huduma zingine .....	9
3.10	Utunzaji wa kumbukumbu na taarifa .....	10
3.11	Mgawanyo wa Majukumu ya wafanyakazi katika Nyumba ya Upataji Nafuu.....	10
3.12	Muundo wa Nyumba za Upataji Nafuu.....	12
3.13	Nyaraka za Usajili .....	12
3.14	Sheria, Kanuni na Taratibu .....	13
3.15	Ukiukwaji wa Taratibu na Kanuni katika Nyumba za upataji nafuu .....	13
4	Viambatisho .....	15
	Kiambatisho I: Usajili wa Mkazi wa Nyumba ya Upataji Nafuu.....	15
	Kiambatisho II: Mkatiba wa Kijiunga na Nyumba ya Upataji Nafuu.....	19
	Kiambatisho III: Medical Examination Form for clients before entering Sober Houses Services.....	22
	Kiambatisho IV: Fomu ya Rufaa .....	23

## **VIFUPISHO**

MoHCDGEC	Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children
MNH	Muhimbili National Hospital
IMC	Ilala Municipal Council
DCEA	Drug Control and Enforcement Authority
CNCDCZ	Commission for National Coordination and Drug Control Zanzibar
DCC	Drung Control Commission
THPS	Tanzania Health Promotion Support
DFT	Drug Free Tanzania
PEDDEREF	People with Drug Dependence Relief Foundation
LHRO	Life & Hope Rehabilitation Organization
TACAIDS	Tanzania Commission for AIDS
VSH	Voice of Sober House
VVU	Virusi Vya Ukimwi
UNODC	United Nations Office On Drugs and Crime
UNAIDS	United Nations Programme on HIV/AIDS
WHO	World Health Organization
DMO	District Medical officer
MMOH	Municipal Medical Officer of Health
RMO	Regional Medical Officer

CMOH

Community Medical Officer of Health

## MISAMIATI

**Uraibu** - Ni hali ya kuathirika kwa ubongo kunakosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya ambapo mtumiaji hujikuta akishindwa kuachana na matumizi ya dawa hizo pamoja na kufahamu madhara yake.

**Kituo cha huduma za awali (Drop in centre)** - Ni sehemu ambayo watumiaji wa dawa za kulevya wanapata huduma za msingi kama unasihi, huduma ya kwanza, usafi, mapumziko na huduma za rufaa.

**Nyumba ya Upataji Nafuu** - Sehemu ambayo watumiaji pombe na dawa za kulevya walioacha matumizi hayo, huwasaidia waraibu ambao bado wako kwenye matumizi ya vilevi kuachana navyo au kupata nafuu kwa kutumia hatua kumi na mbili za upataji nafuu pamoja na unasihi.

**Mtangulizi** - Ni mtu aliye katika unafuu wa muda mrefu ambaye huwaongoza waraibu wapya kuweza kuwapa mbinu mbalimbali zitakazowawezesha kutorudia matumizi ya dawa za kulevya

**Methadone** - Dawa inayotumika kuondoa maumivu kwa waraibu wanaotumia dawa ya kulevya aina ya *heroin*.

**Ustiri wa Mihadarati** - Ni mikutano inayowahusisha watumiaji wenye nia ya kuacha kutumia na walioacha kutumia dawa za kulevya, ambapo washiriki hushauriana na kupeana mbinu za kuishi bila kutumia dawa za kulevya, kwa kutumia hatua 12 za upataji nafuu.

**Hatua 12 za upataji nafuu** - Ni kanuni zilizowekwa kukabiliana na uraibu wa dawa za kulevya

**Wakazi** - Waraibu wanaopata huduma katika nyumba za upataji nafuu

# 1 UTANGULIZI

## 1.1 Matumizi ya Dawa za Kulevya Nchini

Tatizo la matumizi ya dawa za kulevya huathiri afya, uchumi na jamii kwa ujumla. Pombe hutumika zaidi ikifuatiwa na tumbaku, bangi, mirungi, heroin na cocaine. Dawa ya kulevya aina ya heroin imethibitika kuwa na athari zaidi kwa watumiaji, ambapo inakadiriwa kuwa na watumiaji wapatao 200,000 hadi 425,000 na kati yao 20,000 hadi 42,500 wakijidunga dawa hiyo<sup>1</sup>. Kundi linaloongoza kwa matumizi ya dawa za kulevya ni vijana wa umri wa miaka 15 hadi 35. Mikoa inayoongoza kwa matumizi ya dawa za kulevya nchini ni Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Morogoro, Dodoma na Mbeya<sup>2</sup>. Dawa za kulevya hutumika zaidi mijini na sasa zimeanza kutumika kwa kasi kwenye miji midogo na hata vijijini<sup>3</sup>. Utumiaji wa dawa za kulevya mchanganyiko kwa wakati mmoja umeanza kuzoleka hapa nchini, ambapo bangi, *heroin*, pombe, tumbaku na dawa tiba zenye asili ya kulevya kama valium huchanganywa kwa namna mbalimbali.

## 1.2 Athari za Matumizi ya Dawa za Kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya kwa muda mrefu husababisha uraibu, magonjwa ya akili na maradhi mbalimbali. Matumizi ya dawa hizo husababisha vifo vya ghafla, maambukizi ya VVU, homa ya ini, kifua kikuu, magonjwa ya moyo, magonjwa ya mfumo wa hewa na watoto huzaliwa kabla ya muda.

Tabia ya kuchangia vifaa vya kujidungia kama vile sindano mionganoni mwa wajidunga imechangia ongezeko la magonjwa ambukizi ya damu kama vile VVU, homa ya ini aina B na C. Inakadiriwa maambukizi ya VVU mionganoni mwa wajidunga ni asilimia 36 wakati maambukizi ya homa ya ini aina C ni asilimia 75.6<sup>4</sup>. Vilevile, maambukizi hayo yamechangiwa na tabia nyininge hatarishi kama vile ngono zembe. Mara nydingi watumiaji wengi wa dawa za kulevya hukutwa na zaidi ya tatizo moja la kiafya.

Athari zinazosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya katika jamii ni pamoja na watumiaji wa dawa hizo kujihusisha na uhalifu hivyo kuhatarisha usalama wa jamii. Aidha, utupwaji hovyo wa sindano zilizotumika kujidungia dawa za kulevya huhatarisha afya ya jamii pale mtu atakapozikanyaga na kujichoma kwa bahati mbaya au watoto wanapozichezea.

Athari nyininge ambazo huwakumba zaidi wajidunga ni vifo vya ghafla. Watumiaji wengi hasa vijana wamejikuta wakiacha shule na wengine kupoteza ajira. Serikali huingia gharama kubwa

<sup>1</sup> Ministry of Health (2014) Consensus Estimates on key Population Size and HIV Prevalence in Tanzania

<sup>2</sup> DCC (2012) Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchini

<sup>3</sup> UCSF and DCC, 920140 Size Estimation of People who Use Drugs in Tanzania

<sup>4</sup>Nyandindi et al (2013), HIV Serostatus, HCV and Depression among Injection Drug Users in Kinondoni Municipality of Dar es Salaam.

katika kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya. vilevile biashara ya dawa za kulevya huambatana na rushwa hivyo kuathiri utoaji wa haki.

Uzalishaji wa dawa za kulevya husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira hasa kilimo cha bangi na mirungi ambacho huambatana na ukataji hovyo wa misitu ambao huchangia katika uharibifu wa vyanzo vya maji.

### **1.3 Mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya nchini**

Hapo awali nchi haikuwa na huduma maalum za tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya na badala yake walikuwa wanapatiwa tiba pamoja na watu wenye magonjwa ya akili. Hivi karibuni mashirika ya “UNODC, UNAIDS na WHO” yamekuwa yakihamasisha kutumia programu za tiba zilizothhibitika kisayansi kuwasaidia watumiaji wa dawa za kulevya kuweza kuachana na matumizi ya dawa hizo<sup>5</sup>. Hata hivyo, kwa kuwa tiba ya uraibu ni suala mtambuka ambalo huhitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali ili kufikia malengo yake.

Programu hizo ni pamoja na tiba kwa kutumia dawa ya methadone, kuondoa athari ya dawa za kulevya mwilini “*detoxification services*”, vituo vya kutolea huduma za msingi kwa watumiaji wa dawa za kulevya “*drop-in centres*”, huduma za udungaji salama, huduma kwenye Nyumba za Upataji Nafuu na uelimishaji juu ya athari ya matumizi ya dawa za kulevya. Programu hizi zinalenga kupunguza athari zitokanazo na matumizi ya dawa hizo kwa waraibu. Hata hivyo, katika maeneo ambayo hayana huduma hizi, watumiaji wa dawa za kulevya wanashauriwa kwenda kwenye vituo vya huduma za afya.

### **1.4 Nyumba za Upataji Nafuu**

Sehemu ambayo watumiaji pombe na dawa za kulevya walioacha matumizi hayo, huwasaidia waraibu ambao bado wako kwenye matumizi ya vilevi kuachana navyo au kupata nafuu kwa kutumia hatua kumi na mbili za upataji nafuu pamoja na unasihi.

Nyumba hizi za upataji nafuu zinawawezesha waraibu kukaa kwenye mazingira tulivu yasiyoruhusu matumizi ya vilevi vyoyote, ambapo waraibu huishi humo kwa kipindi kisichopungua miezi minne. Wakati wakiwa katika nyumba hizi hufanya kazi mbalimbali za mikono na burudani.

#### **1.4.1 Historia ya Nyumba za Upataji Nafuu Nchini**

Nyumba ya kwanza ya upataji nafuu ilifunguliwa huko Zanzibar mwaka 2009 ikifuatiwa na Tanzania Bara mnamo mwaka 2012. Nyumba za upataji nafuu zinamilikiwa na asasi za kiraia. Nyumba za upataji nafuu hupokea waraibu wa vilevi mbalimbali ikiwemo bangi, *heroin*, pombe na cocaine.

---

<sup>5</sup> WHO, UNODC, UNAIDS (2012) Technical Guide for countries to set targets for universal access to HIV Prevention, treatment and Care for injecting drug users.

#### **1.4.2 Umuhimu wa Mwongozo wa Nyumba za Upataji Nafuu**

Kumekuwa na ongezeko la uanzishaji na uendeshwaji wa Nyumba za Upataji Nafuu bila kufuata taratibu. Hali hiyo imesababisha walengwa kuishi katika mazingira hatarishi ambayo huweza kusababisha maradhi ya kuambukiza kutokana na msongamano, maambukizi ya VVU na mimba zisizotarajiwa kutokana na kuchanganywa wanawake na wanaume, uwezekano wa kuendelelea na matumizi ya dawa za kulevya kutokana na usimamizi hafifu.

Hivyo, kulikuwa na haja ya kuandaa mwongozo utakaoainisha vigezo vitakavyotumika katika usajili, uendeshaji na usimamizi ili kutoa huduma zenyne viwango vinavyokubalika kimataifa kwenye huduma ili kumwezesha mraibu kubaki bila matumizi ya dawa za kulevya.

#### **1.4.3 Kanuni za kuzingatiwa katika Nyumba za Upataji Nafuu**

Taratibu, vigezo na kanuni zifuatazo zilizingatiwa katika utayarishaji wa mwongozo huu ili kusimamia nyumba za upataji nafuu

- a) Usimamizi bora, haki za binadamu kwa kuzingatia tamaduni husika umri na jinsia;
- b) Huduma rafiki kwa gharama nafuu;
- c) Huduma zilenge kujenga afya na ustawi wa wakazi;
- d) Matumizi ya programu za matibabu zilizothibitika kisayansi kuwasaidia watumiaji wa dawa za kulevya ambapo hatua kumi na mbili za upataji nafuu ndio msingi wa utoaji huduma katika nyumba hizo;
- e) Huduma endelevu zenyne kukidhi mahitaji ya upataji nafuu;
- f) Kujijengea uwezo wa kujiongoza; na
- g) Kulenga makundi maalum na mahitaji yao.

## **2 VIGEZO VYA UANZISHAJI NA UENDESHAJI WA NYUMBA ZA UPATAJI NAFUU**

Vifuatavyo ni vigezo vya uanzishaji na uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu.

### **2.1 Miundombinu na Vifaa**

#### **Mahali**

Nyumba iwe kwenye eneo tulivu ambalo liko mbali na eneo shawishi linaloweza kuwarudisha kwenye matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, inashauriwa kuwa karibu na kituo cha afya ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za vipimo na matibabu ya maradhi mbalimbali.

## **Eneo**

Eneo lenye Nyumba ya Upataji Nafuu linatakiwa kuwa na nafasi ya kutosha kuweka michezo mbalimbali na kuwa na eneo la kupumzikia. Aidha, kwenye nyumba zenyenye uwezo wa kuweka sehemu za ufundi stadi zinashauriwa kufanya hivyo.

Jengo liwe safi, lenye mwanga na hewa ya kutosha na vyumba vyenye vyakula wa usiopungua mita 3 kwa mita 3 kwa kila chumba na madirisha yasiyopungua ukubwa wa mita 1.5 kwa mita 2. Kuwe na ofisi, chumba cha mikutano kitakachotosheleza kila mkazi kushiriki mkutano akiwa amekaa kwa uhuru.

## **Eneo la malazi**

Inashauriwa kuwa na nafasi ya kutosha kati ya mtu mmoja na mwingine katika malazi ili kuondoa msongamano. Vipimo vinyoyoshauriwa angalau mita za ukubwa 3 (mita 2 x mita 1.5) wa eneo la mzunguko.

## **Ofisi**

Kila Nyumba ya Upataji Nafuu inatakiwa kuwa na ofisi.

## **Sebule**

Kuwe na chumba kikubwa kwa ajili ya wakazi kuweza kukaa kwa nafasi na kupumzika

## **Paa**

Jengo liwe na paa lisilovuja na dari zilizo katika hali nzuri

## **Vitanda**

Kuwe na idadi ya kutosha ya vitanda vyenye vyandarua na viwe umbali usiopungua sentimita 60 au futi mbili kati ya kitanda kimoja na kingine ili kutoa njia kwa watumiaji wa vitanda. Kila Kitanda kimoja alale mtu mmoja, hairuhusiwi kulala zaidi ya mtu mmoja kwenye kitanda kimoja.

## **Vyoo na mabafu**

Choo kimoja na bafu moja vitumike na watu wasiozidi 12 na viwe safi muda wote.

## **Eneo la kufulia**

Kuwe na eneo maalum kwa ajili ya usafi wa nguo na kila mkazi aweze kulitumia.

## **Jiko na sehemu ya kulia chakula**

Kuwe na sehemu ya jiko, vyombo vya kutosha na sehemu ya kuhifadhi vyakula. Aidha, kuwe na eneo la kulia chakula linalotosheleza kuepuka wakazi kula chakula kwenye vyumba vya kulala.

### **Stoo**

Jengo liwe na eneo la kuhifadhi vifaa vya nyumba.

### **Maji**

Kuwe na maji salama, yanayotosheleza mahitaji na kupatikana muda wote

### **Ukuta**

Jengo liwe na ukuta unaozunguka kwa ajili ya ulinzi na kudhibiti uingiaji na utokaji wa watu. Kwa nyumba zilizo katika makazi ya watu wengi ukuta ujengwe kwa matofali.

### **Samani**

Ziwe zinazosafishika kirahisi na ziwe safi muda wote bila kuharibika kwa urahisi kuchanika/kubomoka au kuhatarisha watumiaji.

### **Mahitaji mengine**

Kuwe na machapisho yakiwemo hatua 12 za upataji nafuu na kabati au mahali yatakapohifadhiwa na rahisi kuyaona na kuyatumia, kuwe na ubao wa kuandika kwenye chumba cha mikutano hususani ubao mweupe na kalamu zake (*white board and marker pens*), viti na meza za kutosha, mikeka, daftari za kuandikia na kalamu.

## **2.2 Watoa huduma**

Watoa huduma wawe wa aina mbili; viongozi na wahudumu. Watoa huduma wathibitishwe kuwa na afya. Katika nyumba kutakuwa na wafanyakazi wafuatao:- meneja wa nyumba, mtangulizi wa hatua 12 za upataji nafuu ambao watasimamia programu ya upataji nafuu na wahudumu wanaosimamia upatikanaji wa mahitaji ya kila siku ya wakazi wa nyumba kama chakula na usafi. Majukumu ya kila mtoa huduma yameainishwa.

## **2.3 Aina za huduma zinazotolewa**

Nyumba za Upataji Nafuu hutoa huduma mbalimbali katika kumwezesha mraibu kupata stadi za maisha zitakazomwezesha kufanikiwa kuachana na matumizi ya vilevi.

### **2.3.1 Huduma ya saikolojia – Jamii (*psychosocial services*)**

Huduma hizi zinaweza kutolewa na watumiaji waliopata nafuu kwa muda mrefu au wataalam wa unasihi:

- Vikundi vya kusaidiana (*peer support*);
- Unasihi kwa mtu binafsi au vikundi 1; na
- Huduma nyingine zilizothibitishwa kisayansi kuwasaidia waraibu.

### **2.3.2 Huduma ya kwanza**

Kila nyumba ya upataji nafuu inatakiwa kuwa na kisanduku cha huduma ya kwanza.

### **2.3.3 Huduma ya rufaa**

Rufaa itolewe pale mraibu anapokuwa na magonjwa ya akili, ugonjwa wa kifua kikuu, magojwa ya zinaa, malaria pamoja na mahitaji ya kisheria. Mraibu asindikizwe kwa kutumia fomu husika kama ilivyoainishwa (**Kiambatisho IV**).

### **2.3.4 Chakula na malazi**

- a) Wapate milo isiyopungua mitatu kwa siku yenye wanga, protini, mboga za majani na matunda
- b) Ratiba inayoruhusu walau saa sita za kulala usiku na muda wa kupumzika mchana

Aidha, katika kufanikisha lengo la upataji nafuu, nyumba hizi zinatakiwa kutoa huduma nyingine kama ifuatavyo:-

- a) Michezo na burudani;
- b) Tafakuri (*meditation*); na
- c) Stadi za Maisha.

## **2.4 Usalama na dharura**

Nyumba za Upataji Nafuu lazima ziwe salama kwa wakazi wake. Usalama huo uzingatie yafuatayo:-

### **Udhibiti wa moto**

Nyumba za Upataji Nafuu zinatakiwa kuchukua tahadhari katika kukabiliana na moto. Tahadhari hizo ni pamoja na kuzuia, kupunguza na kudhibiti moto ambao unaweza kusababisha athari kama vile ucharibifu wa mali, majeraha na vifo. Tahadhari hizo ni kama zifuatazo:-

- a) Uwepo wa viashiria moto na vifaa vya zimamoto;
- b) Milango yote ifunguke kwa kuelekea nje na kuwe na alama inayoelekeza njia ya kutoka/kujiokoa;
- c) Kuwe na vifaa vya zimamoto (*fire extinguishers*) vilivyothibitishwa na mamlaka husika, na viwekwe mahali rahisi kufikika na wakazi waelimishwe namna ya kuvitumia;
- d) Vifaa na kemikali zinazoweza kulipuka (*vilipuzi*) kama gesi, petroli, dawa za kuua wadudu vihifadhiwe au kutupwa sehemu salama;
- e) Epuka msongamano katika nyumba unaozidi idadi inayotakiwa;
- f) Ukaruzi wa nyumba ufanyike mara kwa mara ili kubaini mianya inayoweza kusababisha moto;
- g) Kuwe na namba ya mawasiliano ya simu ya dharura inayofahamika kwa wakazi wa nyumba. Tumia vitu visivyoshika moto kirahisi. Wakazi wapate mafunzo ya kukabiliana na janga la moto;
- h) Taratibu zinazotolewa na mamlaka ya udhibiti wa janga la moto zifuatwe; na

- i) Endapo moto utatokea msaada utolewe kwa wakazi wasioweza kujiokoa.

#### **Usalama wa mali za wakazi wa nyumba**

- a) Hakikisha usalama wa wakazi na mali zao;
- b) Kuwe na utaratibu wa upokeaji wa wageni na wakazi kwenye nyumba;
- c) Silaha na vifaa hatarishi visiruhusiwe ndani ya nyumba; na
- d) Kuwe na mikakati madhubuti ya kuhakikisha wakazi hawanyanyaswi kimwili, kisaikolojia wala kingono.

### **2.5 Utupaji takat**

Nyumba iwe na mfumo wa utupaji takat usioathiri mazingira kwa namna yoyote.

## **3 UANZISHAJI NA UENDESHAJI WA NYUMBA ZA UPATAJI NAFUU**

### **3.1 Umiliki**

Mtu yeote binafsi au Taasisi anaweza kuanzisha na kuendesha Nyumba ya Upataji Nafuu kwa waathirika wa dawa ya kulevya.

### **3.2 Ithibati ya uanzishwaji wa Nyumba za Upataji Nafuu**

Huduma ya Nyumba ya Upataji Nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya haitaanzishwa isipokuwa kwa idhini ya Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania Bara. Hati ya Kibali itatolewa tu baada ya kukidhi vigezo vinavyohitajika kama ilivyoelezwa katika Mwongozo huu na kanuni zingine husika za kitaifa. Mchakato wa kutoa idhini utahusisha ukaguzi wa nyumba na uhakiki wa hati zote zilizolekezwa kwenye Mwongozo.

Tathmini ya ukaguzi itatoa madaraja matatu ya uanzishaji na uendeshaji wa nyumba hizo; 1) Inakubalika; 2) Inahitaji maboresho, 3) Haikubaliki.

- a) **Inakubalika** - Maana yake ni kwamba nyumba hiyo imekidhi vigezo vinavyohitajika katika uanzishaji na uendeshaji wa nyumba ya upataji nafuu baada ya kujaza maombi fomu namba moja, ambayo inapatikana katika tovuti ya Mamlaka ([www.dcea.go.tz](http://www.dcea.go.tz)), hivyo kibali kitatolewa, Hati ya idhini yakuendesha nyumba ya upataji nafuu itadumu kwa kipindi cha miaka mitatu.
- b) **Inahitaji maboresho** - Inamaanisha kwamba, nyumba hiyo inakidhi baadhi ya vigezo, lakini inahitaji kufanyiwa marekebisho. Iwapo nyumba hiyo haina wakazi mmiliki atatakiwa afanye marekebisho yanayohitajika kabla ya kupewa idhini. Iwapo nyumba hiyo ina wakazi atapewa muda wa miezi mitatu kufanya marekebisho yanayohitajika.

Ikiwa atashindwa kufanya marekebisho hayo katika kipindi hicho kibali chake kitasitishwa na wakazi wake watahamishiwa kwenye nyumba nyingine.

- c) **Haikubaliki** - Maana yake ni kwamba, nyumba hiyo haijakidhi vigezo vinavyokubalika au haiendani kabisa na maelezo ya Mwongozo na masharti yake. Mmiliki hatapewa hati ya idhini isipokuwa anaweza kuwasilisha upya maombi yanayokidhi vigezo vya Mwongozo.

### **3.3 Utaratibu wa kupata Cheti cha idhini**

Utaratibu wa kupata cheti cha idhini utasimamiwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta.

Nyumba zilizoidhinishwa zitatemebelewa mara moja kwa mwaka au kila itakapoonekana umuhimu wa kufanya hivyo na Ofisi ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta au Taasisi nyingine za Serikali. Mmiliki wa nyumba ambaye hatakubaliana na matokeo ya ukaguzi anaweza kukata rufaa kwa Katibu Mkuu anayehusika na masuala ya udhibiti wa dawa za kulevyta. Aidha, usajili ya Nyumba ya Upataji Nafuu hauhamishiki, iwapo huduma itahamia kwenye nyumba nyingine usajili ufanyike upya.

### **3.4 Utaratibu wa kufutiwa utoaji huduma**

Huu ni utaratibu wa kufutiwa utoaji huduma za uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu kufuatia kukiukwa kwa masharti na kanuni zilizoainishwa katika Mwongozo huu.

Kufutiwa Cheti cha idhini kutahusisha nyumba ambayo baada ya tathmini itabainika kupata hati ya *Haikubaliki* au Inahitaji kuboreshwa mara tatu mfululizo. Nyumba ambayo idhini yake imefutwa, itapewa muda wa mwezi mmoja kuwahamisha wakazi wake kwenye huduma nyingine ya upataji nafuu au nyumba za upataji nafuu nyingine.

### **3.5 Kusitisha utoaji huduma kwa hiari**

Nyumba yejote ya upataji nafuu inayokusudia kusitisha huduma zake, kabla ya kufanya hivyo itapaswa kutoa taarifa kwa Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa ya Kulevyta, Tanzania Bara. Taarifa ya kukusudia kusitisha huduma sharti ieleze sababu za kusitisha huduma na namna ya kuwahamisha wakazi wake kwenye nyumba nyingine za upataji nafuu.

### **3.6 Uongozi katika Nyumba ya Upataji Nafuu**

Nyumba ya Upataji Nafuu inatakiwa kuendeshwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Taratibu hizo zitazingatia dira, dhima, madhumuni na njia za kutatua migogoro inayoweza kujitokeza. Sheria, kanuni na taratibu hizo lazima ziwezeshe wakazi wake kujinasua na dawa za kulevyta na kuwajengea tabia njema. Taratibu hizo zieleweke kwa wakazi na watoa

huduma na kuwekwa mahali pa wazi kwa urahisi wa rejea. Aidha, haki na wajibu wa wakazi na watoa huduma zitazingatiwa.

Nyumba ya Upataji Nafuu itakuwa na mfumo wa uongozi ulioainishwa vizuri ili kusimamia utoaji wa huduma. Hii itajumuisha uwepo wa Mmiliki/Mtawala na watumishi wengine ikiwemo timu ya huduma kwa wateja inayoongozwa na Meneja wa nyumba. Nyumba inayopata misaada kutoka kwa Taasisi zingine, itahakikisha kuna uwazi na kuwa na matumizi mazuri ya rasilimali fedha. Taarifa za matumizi ya fedha lazima ziandikwe vizuri kwa madhumuni ya kukaguliwa wakati wowote itakapohitajika.

### **3.7 Utaratibu wa kujiunga na nyumba za upataji nafuu**

Vigezo vifuatavyo vitazingatiwa wakati wa kusajili wakazi wapya:

- a) Kujiunga na huduma kutakuwa ni kwa hiari;
- b) Mraibu lazima awe raia wa Tanzania. Raia wa kigeni wenye vibali halali vya kuishi nchini wanaweza kukubalika;
- c) Waraibu walio na umri chini ya miaka 18 hawataruhusiwa kuishi pamoja na watu wazima katika nyumba moja. Sheria zinazohusu watoto zitazingatiwa;
- d) Waraibu wa kiume na wa kike hawaruhusiwi kusajiliwa/ kuishi katika nyumba moja ya upataji nafuu;
- e) Kabla ya kupokelewa kwenye Nyumba ya Upataji Nafuu mraibu lazima afanyiwe uchunguzi wa magonjwa ya afya ya akili na magonjwa ya kuambukizwa. Fomu kwa ajili ya kupima hali ya afya zitapatikana katika Nyumba za Upataji Nafuu, au katika kituo cha Afya kilicho karibu. Uchunguzi wa afya utafanywa na Tabibu kutoka katika kituo cha kutolea huduma cha Serikali na taarifa ya uchunguzi itawasilishwa kwenye nyumba ya upataji nafuu kwa kutumia fomu zilizojazwa kikamilifu (**Kiambatisho III**); na
- f) Kabla ya mraibu kusajiliwa/kupokelewa atafanyiwa udahili kwa kutumia fomu maalum (**Kiambatisho I**) na atasaini Mkataba (**Kiambatisho II**).

### **3.8 Usimamizi Shirikishi na Uhakiki wa Ubora wa Huduma**

Usimamizi shirikishi na uhakiki wa ubora wa huduma utafanyika wakati wowote ili kufuatilia ubora wa huduma zinazotolewa katika nyumba za upataji nafuu. Usimamizi huo utafanywa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa kushirikiana na Taasisi nyingine pale inapohitajika.

### **3.9 Kuunganishwa na huduma zingine**

Kwa kuwa watu waliopo katika hali ya upataji nafuu wana mahitaji mengi, wakati mwingine watahitaji kupata huduma maalum ili kutatua masuala yanayowakabili. Nyumba ya Upataji Nafuu inapaswa kuwa na utaratibu wa namna ya kuwaunganisha waraibu na huduma nyingine za ziada. Mfano kwa waraibu wenye matatizo ya kiafya watapewa rufaa kwenda kwa wataalam wa Afya kwa kutumia fomu maalum (**Kiambatisho IV**).

### **3.10 Utunzaji wa kumbukumbu na taarifa**

Kumbukumbu za wakazi wote lazima zitunzwe katika sehemu maalum yenye usalama. Mmiliki wa nyumba lazima atunze kumbukumbu muhimu za kila mkazi kama vile:-

- a) Taarifa za msingi za mkazi na mawasiliano yake wakati wa tahadhari;
- b) Historia ya matumizi ya dawa za kulevy;
- c) Kumbukumbu za nyuma za uhalifu;
- d) Historia ya magonjwa; na
- e) Mkataba wa Mkazi.

Aidha, ni lazima pawepo taarifa ya mahesabu kwa malipo ya ada zinazopokelewa kutoka kwa kila mkazi, leja moja yenye orodha ya wakazi wanaojiunga na wanaoondoka. Leja ihusishe maelezo ya rufaa yaliyosababisha wakazi kujiunga na huduma na mazingira yaliyomfanya aondoke kutoka kwenye nyumba. Nyumba zitahifadhi taarifa za mraibu sio chini ya miaka mitano baada ya mraibu kuacha kupata huduma.

Kila Nyumba ya Upataji Nafuu inatakiwa kutoa taarifa kila robo mwaka. Taarifa hizo zitakuwa na viashiria kama vinavyoonekana katika fomu namba tatu inayopatikana katika tovuti ya Mamlaka Taarifa hizo zitawasilishwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy.

### **3.11 Mgawanyo wa Majukumu ya wafanyakazi katika Nyumba ya Upataji Nafuu**

Nyumba za Upataji Nafuu zinatoa huduma mbalimbali ambazo huhitajika kuainishwa bayana ili kupunguza muingiliano kwa watoa huduma wakati wa utekelezaji. Majukumu hayo yameainishwa kama ifuatavyo:

#### **(a) Mmiliki/Msimamizi**

##### **Sifa**

Ni mtu yejote au taasisi yoyote

##### **Wajibu**

- a) Kuwajibika katika mamlaka za juu;
- b) Msemaji mkuu katika Nyumba ya Upataji Nafuu;
- c) Kuandaa na kutoa taarifa za mradi kwa taasisi husika; na
- d) Kuunganisha wakazi na huduma nyingine.

**(b) Meneja wa Nyumba ya Upataji Nafuu**

**Sifa**

- a) Mtu yoyote aliye na utaalam na uzoefu wa kufanya kazi na waraibu kwa takribani miaka miwili; na
- b) Kuwa na uelewa wa hatua 12 za upataji nafuu inafaa Zaidi.

**Majukumu ya Meneja wa Nyumba ya Upataji Nafuu**

- a) Kufanya udahili wa waraibu wapya;
- b) Kuratibu mafunzo ya wafanyakazi na wanaojitolea;
- c) Uangalizi wa shughuli za uendeshaji nyumba ukiwemo usafi;
- d) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa kanuni na taratibu za nyumba;
- e) Kuwasiliana na familia kuhusu mwenendo wa mraibu;
- f) Usuluhishi wa migogoro ya ndani ya nyumba;
- g) Kuwakilisha na kutetea ustawi wa nyumba pale inapohitajika;
- h) Kuhakikisha usalama wa nyumba na wanaoishi; na
- i) Kuwaunganisha wakazi wa nyumba ya upataji nafuu na huduma zingine.

**(c) Mtangulizi wa Hatua 12 za upataji nafuu**

**Sifa**


- a) Mtu aliye katika upataji nafuu, mwaminifu na mwajibikaji;
- b) Aliyeacha kutumia dawa za kulevyaa angalau kwa mwaka mmoja; na
- c) Aliye na ufahamu na uzoefu kuhusu hatua 12 za upataji nafuu.

**Wajibu**

- a) Kuratibu mikutano ya makundi ya upataji nafuu na mtu mmoja mmoja;
- b) Kuhakikisha vipindi vyaa asubuhi vyaa kujitambua vinaendeshwa kwa usahihi;
- c) Kuratibu mikutano ya usitiri wa mihadarati na pombe;
- d) Kuwaongoza wakazi ambao ni wageni; na
- e) Kutoa taarifa ya mienendo ya kila siku ya waraibu kwa Meneja wa Nyumba.

### **3.12 Muundo wa Nyumba za Upataji Nafuu**

Muundo wa Nyumba za Upataji Nafuu ni kama ulivyoainishwa hapo chini:



### **3.13 Nyaraka za Usajili**

Nyaraka zifuatazo lazima ziambanishwe katika Fomu ya Maombi ya usajili wa Nyumba za Upataji Nafuu:-

1. Nakala za vyeti vya taaluma;
2. Nakala ya hati ya usajili wa asasi/kampuni;
3. Nakala ya katiba;
4. Maoni kutoka kwa uongozi wa Kata ilipo Nyumba ya Upataji Nafuu;
5. Wasifu wa msimamizi na meneja wa nyumba;
6. Mgawanyo wa majukumu;
7. Ratiba (kwa siku, kwa wiki, kwa mwezi);

8. Sheria za nyumba kwa ajili ya wakazi;
9. Vigezo vya kuwapokea na kuwaruhusu wakazi;
10. Muundo wa uongozi wa wafanyakazi;
11. Mpango kazi na bajeti;
12. Mkataba wa kupanga nyumba wa mwaka mmoja au zaidi/hati ya umiliki wa nyumba; na
13. Maelezo ya Mradi/Andiko.

### **3.14 Sheria, Kanuni na Taratibu**

Nyumba za Upataji Nafuu lazima ziwe na sheria, kanuni na taratibu za kuishi katika nyumba husika kama ifuatavyo:-

1. **Haki za Binadamu:** Kila mraibu anastahili kupata haki za msingi za kibinadamu. Hairuhusiwi kwa mraibu yeoyote kunyimwa huduma kutokana na tofauti za kabilia, dini, rangi, uraia au hali ya kiafya.
2. **Mazingira:** Kanuni na taratibu za usafi wa mazingira zizingatiwe katika uendeshaji wa nyumba za upataji nafuu.
3. **Jinsi:** Nyumba ya Upataji Nafuu hairuhusiwi kuwa na watu wa jinsi tofauti.
4. **Tamaduni:** Tofauti za tamaduni za wakazi zizingatiwe na kuheshimiwa.
5. **Unyonyaji:** Marufuku kwa mkazi yeoyote kuhuishwa na shughuli zozote za kinyonyaji kama vile kutumikishwa kingono au kufanyishwa kazi kwa manufaa yasiyo ya wakazi.
6. **Usiri:** Hairuhusiwi kutoa taarifa binafsi ya mkazi yeoyote isipokuwa kwa mujibu wa sharia.
7. **Gharama za Huduma:** Kila nyumba inatakiwa kuainisha bayana gharama ya huduma zinatolewa. Gharama hizo ni pamoja na ada, fedha za tahadhari na marejesho. Taarifa hizi zinaweza kukaguliwa wakati wowote na wakaguzi wa nje kila itakapohitajika.
8. **Uhalifu:** Hairuhusiwi kwa mkazi yeoyote kujihusisha na vitendo vya kihalifu.
9. **Malalamiko:** Malalamiko, madai au mashauri ya kisheria ambayo hayawezi kutatuliwa katika ngazi ya nyumba yapelekwe katika ngazi husika.
10. **Tiba:** Hairuhusiwi kutoa huduma za tiba katika nyumba ya upataji nafuu isipokuwa huduma ya kwanza tu. Huduma za tiba zinatolewa na kituo cha afya kilicho karibu kwa kusindikizwa na watoa huduma wa Nyumba ya Upataji Nafuu. Kwa wagonjwa watakaopatiwa dawa ambazo watazipata kutoka vituo vya huduma ya afya, dawa hizo zitahifadhiwa na kutolewa na Meneja wa Nyumba husika.

Nyumba yoyote itakayokiuka sheria, taratibu na kanuni za uendeshaji huduma ya upataji nafuu itapewa adhabu kali ikiwemo kufungiwa utoaji huduma.

### **3.15 Ukiukwaji wa Taratibu na Kanuni katika Nyumba za upataji nafuu**

Mambo yafuatayo ni ukiukwaji wa kanuni na taratibu katika Nyumba za Upataji Nafuu:

1. Matumizi ya dawa za kulevya na pombe;
2. Umiliki wa silaha na vifaa hatarishi;
3. Kujihusisha na uhalifu;

4. Vurugu na vitendo vya uharibifu;
5. Wizi; na
6. Kufanya ngono katika nyumba ya upataji nafuu.

Yeyote atakayekiuka taratibu na kanuni hizi attachukuliwa hatua kali za kinidhamu.

## **4 Viambatisho**

### **Kiambatisho I: Usajili wa Mkazi wa Nyumba ya Upataji Nafuu**

#### **MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

#### **USAJILI WA MKAZI WA NYUMBA YA UPATAJI NAFUU**

##### **1. TAARIFA BINAFSI**

..... Jina la kwanza ..... Jina la katii ..... Jina la ukoo  
Jina maarufu: (a.k.a.) .....

Tarehe ya kuzaliwa: .....

Jinsia: Mwanaume/Mwanamke

Dini: .....

Kabila: .....

Namba na aina ya kitambulisho: .....

##### **Anuani:**

Mtaa: ..... Kata: .....

Wilaya: ..... Mkoa: .....

##### **Taarifa za Mawasiliano**

Namba ya simu anapoishi (nyumbani): .....

Namba ya simu ya mkononi: 1 ..... 2. .....

Barua pepe : .....

Ndoa: Ameoa/Ameolewa; Hajaoa/Hajaolewa; Mtalaka; Ametengana.

Idadi ya watoto: .....

Kiwango cha elimu: .....

Taaluma/Fani: .....

Kazi/Ajira: .....

Muonekano wa mwili: Ana ulemevu .....; Hana ulemavu .....  
(Fafanua).....

## 2. MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

(a) Historia ya Matumizi

Aina ya dawa	Umri wa kuanza matumizi	Njia/Namna ya kutumia

Mengineyo: .....

## 3. TAARIFA ZA TIBA YA URAIBU

(a). Je, uliwahi kupata tiba ya uraibu wa dawa za kulevya?

Ndio: ..... Hapana: .....

Kama Ndio: Jibu maswali yote hapa chini. Kama hapana Jibu: 4, 5,6 na 7.

(b) Historia ya tiba:

Mwaka	Mahali	Aina ya Matibabu	Muda bila Matumizi ya dawa

(c) Sababu za kurudia matumizi ya dawa ya dawa za kulevya:

.....  
.....

(d) Sababu za kuhitaji tiba

.....  
.....

#### **4. TAARIFA ZA UHALIFU**

Je, uliwahi kuhukumiwa, kushikiliwa au kufungwa? Ndio  pana

Ikiwa Ndio,

(Elezea).....  
.....

#### **5. HISTORIA YA TIBA YA MAGONJWA MENGINE**

Je una historia ya magonjwa mengine kama vile? (*Weka ndio au hapana*)

(a) VVU/UKIMWI: .....

(b) Homa ya Ini B/C: .....

(c) Kisukari: .....

(d) Shinikizo la damu: .....

(e) Kifua Kikuu: .....

(f) Ugonjwa wa Akili: .....

(g) Mengine: .....

#### **6. MTU WA KARIBU WA KUMPA TAARIFA**

Jina la Kwanza

Jina la Kati

Jina la Mwisho

Uhusiano: .....

Anuani: .....

Mtaa: ..... Kata: .....

Wilaya: .....Mkoa: .....

**Mawasiliano:**

Simu ya Nyumbani: ..... Simu ya Mkononi: .....

Barua pepe: .....

**7. MDHAMINI**

Jina: .....

Jina la Kwanza: ..... Jina la Kati: ..... Jina la Mwisho: .....

Uhusiano: .....

Anuani: .....

Mtaa: ..... Kata:..... Wilaya: ..... Mkoa: .....

Mawasiliano:

Simu ya Nyumbani: .....Simu ya Mkononi: .....

Barua pepe: .....

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU**

Namba ya Mkazi: .....

Imepokelewa na:-

Jina: ..... Cheo: .....

Sahihi: ..... Tarehe: .....

## **Kiambatisho II: Mkataba wa Kujiunga na Nyumba ya Upataji Nafuu**

**MKATABA** huu unafanyika leo tarehe.....mwezi.....20.....

### **KATI YA**

.....(Jina la nyumba)      wa S. L. P .....Kata  
ya.....Wilaya                ya.....Mkoa                wa  
.....(akijulikana kama “**Meneja**”) kwa upande mmoja;

### **NA**

Bwana/Bi./Bibi ..... (Mkazi wa Nyumba) wa S. L. P  
..... Kata        ya ..... Wilaya        ya  
..... Mkoa wa ..... (akijulikana kama  
“**Mkazi**”) kwa upande wa pili.

Pande zote mbili zinakubaliana yafuatayo:

#### **1. Lengo**

Ni kumwezesha mraibu kupitia hatua 12 za upataji nafuu ili kuachana na matumizi ya dawa za kulevyta. Dhamira ni kuwa na makubaliano ya pamoja ya hiyari kati ya pande mbili ambazo kila moja inakubali kuwa na wajibu wa kufanikisha kile walichokubaliana.

#### **2. Wajibu**

##### **(a) Meneja**

- Kutoa huduma za upataji nafuu kwa kiwango kinachokubalika.
- Kulinda maslahi ya mkazi wa Nyumba.

##### **(b) Mkazi**

- Kufuata sheria, kanuni na taratibu.
- Ushiriki kwa vitendo katika huduma za upataji nafuu.

#### **3. Taratibu**

- Mkazi haruhusiwi kuwa na silaha au vifaa hatarishi.
- Mkazi lazima aheshimu wakazi wenzake.
- Shughuli zinazofanyika ndani hazitakiwi kujadiliwa nje ya Nyumba.
- Mkazi atafukuzwa iwapo atakiuka taratibu za nyumba
- Mkazi atawajibika kumaliza majukumu aliyopangiwa.

- (f) Mkazi hatakiwi kupiga kelele zitakazoleta usumbufu.
- (g) Hairuhusiwi kula chakula kwenye vyumba vyakulala.
- (h) Hairuhusiwi kuvuta sigara.
- (i) Hairuhusiwi kunywa pombe au dawa za kulevya.
- (j) Wakazi wasijihushe na mapenzi.
- (k) Vyumba vinaweza kukaguliwa wakati wowote.
- (l) Usafi wa nyumba na mazingira yake ukamilike kwa wakati
- (m) Hairuhusiwi kwa mkazi ye yeyote kutunza dawa chumbani.

#### **4. Kanuni**

Mkazi anapowasili katika Nyumba ya Upataji Nafuu

- (a) Atafanya udahili na atasaini mkataba (**Kiambatisho I & II**)
- (b) Atapeleka cheti cha vipimo kutoka kwa daktari
- (c) Atasoma na kusaini Mkataba wa Kuishi katika Nyumba ya Upataji Nafuu
- (d) Mkazi anawenza kupimwa iwapo anatumia dawa za kulevya au kileo/pombe
- (e) Atalipa jumla ya shilingi ..... kama ifuatavyo:-

  - Shilingi ..... za tahadhari ambazo zitarejeshwa kulingana na masharti yaliyopo.
  - Shilingi ..... za ada za miezi ..... kwa ajili ya makazi.

- (f) Ataanza kwa kuishi siku 90 za majaribio

#### **Siku 90 za muda wa majaribio**

- (a) Mkazi wa Nyumba hataruhusiwa kutembelewa na mtu ye yeyote isipokuwa kwa ruhusa au idhini ya meneja wa nyumba.
- (b) Mkazi hatoruhusiwa kuwa nje ya Nyumba katika kipindi hicho.
- (c) Mkazi anatakiwa kusaini pindi anapotoka au kurejea kwenye nyumba.
- (d) Mkazi lazima awe na mdhamini.
- (e) Kila mkazi atafanyiwa vipimo vya matumizi ya dawa za kulevya na pombe.
- (f) Mkazi anatakiwa kusaini mahudhurio ya mikutano ya dawa za kulevya na pombe isiyopungua 90.
- (g) Wakazi wenyewe simu watazikabidhi kwa Meneja kipindi cha majaribio na zitatumika kwa sababu maalum.
- (h) Matumizi ya simu binafsi hayataruhusiwa ndani ya siku 90 za majaribio

#### **Baada ya siku 90 za majaribio**

Baada ya siku 90 za majaribio, mkazi anatakiwa kuhudhuria mikutano isiyopungua 6 kwa wiki.

## **Dawa**

- Mkazi hatakiwi kutumia dawa tiba isipokuwa kwa ushauri wa daktari.
- Dawa zihifadhiwe katika maeneo maalum.

### **Muda wa kulala usiku**

- Jumatatu hadi Ijumaa: muda ni saa 4 kamili usiku.
- Jumamosi na Jumapili: muda ni saa 5 kamili usiku.

## **Wageni wanaotembelea Nyumba za Upataji Nafuu**

- Wageni wote lazima waruhusiwe na Meneja.
- Wageni wote lazima wakaguliwe kudhibiti uingizaji wa pombe, dawa za kulevya, silaha na vifaa hatarishi.

### **5. Hatua za kinidhamu**

Hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa yeoyote atakayekiuka taratibu na kanuni zilizowekwa.

### **6. Tarehe na saini ya Mkataba kutumika**

Mkataba huu utaanza kutumika mara utakaposainiwa na **Afisa Muidhiniwa wa Nyumba ya Upataji Nafuu na Mkazi mtarajiwa**. Utatumika kuanzia siku ya tarehe.....  
Mwezi..... Mwaka .....

Pande zote mbili zimekubaliana na kusaini kama inavyoonesha hapa chini:

#### **Meneja wa Nyumba**

Jina: .....

Saini: .....

Cheo: .....

Tarehe: .....

#### **Mkazi**

Jina: .....

Saini: .....

Tarehe: .....

#### **Shahidi**

Jina: .....

Saini: .....

Cheo: .....

Tarehe: .....

#### **Mzazi/Mlezi**

Jina: .....

Saini: .....

Tarehe: .....



## **5 Kiambatisho IV: Fomu ya Rufaa**

Tarehe: .....

Kutoka: .....

Kwenda:.....

Jina la Mkazi: .....

Jinsia:.....

Umri: .....

Sababu ya kupata rufaa: .....

(Kama alikuwa kwenye matibabu aoneshe kwa daktari dawa anazotumia, aina ya matibabu, cheti cha daktari n.k.)

Jina la mtu aliyetoa rufaa.....Saini.....Mhuri.....

### **Mrejesho:**

Jina la Taasisi .....

Maelezo/huduma aliyopewa.....

Tarehe ya kurudi .....

Jina na Cheo cha mto huduma .....

Saini..... Mhuri.....

Tarehe.....